



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



MWALIKO WA WATAZAMAJI WA

**UCHAGUZI MDOGO KATIKA JIMBO LA NGORONGORO NA
KATA YA NAUMBU HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Ngorongoro, Mkoa wa Arusha na Kata ya Naumbu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara tarehe 11 Disemba, 2021.

Kwa mujibu wa kanuni ya 18 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kualika na kusajili watazamaji wa uchaguzi wanaotaka kutazama uchaguzi.

Kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka Taasisi na Asasi mbalimbali nchini ambazo zinahitaji kutazama uchaguzi mdogo katika Jimbo la Ngorongoro, Mkoa wa Arusha na Kata ya Naumbu, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara katika Mkoa wa Mtwara.

Taasisi na Asasi zenye nia ya kutazama uchaguzi huo zinatakiwa kuwasilisha maombi kwa kutumia Mfumo wa Menejimenti ya Watazamaji (OMS) kwa kutumia "link" ifuatayo <https://oms.nec.go.tz>.

Barua ya maombi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuainisha mambo yafuatayo-

- i. Anuani kamili ya Taasisi au Asasi husika;
- ii. Mahali ambapo Taasisi au Asasi husika inafanyia kazi (Physical address);

- iii. Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi au Asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;
- iv. Sehemu ambazo Taasisi au Asasi inataka kufanya zoezi hilo la utazamaji;
- v. Idadi ya watu ambao Taasisi au Asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao;
- vi. Majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi au Asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili;
- vii. Ikiwa Taasisi au Asasi inahusisha watendaji wa kimataifa, wawili angalau wawe Watanzania;
- viii. Kuambatisha nakala au kivuli cha hati ya usajili wa Taasisi au Asasi husika; na
- ix. Kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya Taasisi au Asasi husika.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31 Oktoba, 2021.

Imetolewa leo tarehe...22/10/2021... na:



Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI